## *Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yasogeza zaidi huduma za Ushauri wa kisheria karibu na Wananchi*

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 59(3) na Kifungu cha 8 (a) cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Sura ya 268, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye mwenye mamlaka na dhamana ya kuishauri Serikali katika masuala yote ya kisheria.

Kutokana na changamoto za utawala wa sheria zinazojitokeza, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeandaa Mwongozo wa Huduma za Ushauri wa Kisheria katika Mikoa na Wilaya. Mwongozo huo unaanzisha Kamati za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya ambazo uanzishwaji wake na utendaji kazi wake umeelekezwa katika Mwongozo huo.

Mwongozo huo pamoja na Kamati hizo, vilizinduliwa na Mhe.Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika tarehe 21 Machi 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma. Kamati za Ushauri wa Kisheria zitafanyika katika maeneo ambayo yatapangwa na Kamati za Ushauri wa Kisheria kwa ngazi za Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashiriki katika kuziwezesha Kamati za Ushauri ngazi za Mikoa. Kamati hizi za Mikoa zitasaidia kuzijengea uwezo kamati za Wilaya katika kuendesha kliniki za kisheria. Kamati za wilaya zitafanya kliniki katika ngazi za Tarafa na Kata.

Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kushirikiana na na wadau wengine katika kuziwezesha kamati hizo kuweza kufanya kazi ya kuhudumia wananchi kwa ufanisi zaidi. Wadau hao ni Wizara ya Katiba na Sheria, OR-TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Tume ya Utumishi wa Walimu, Chama cha Mawakili wa Serikali, Chama

cha Mawakili Tanganyika, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza pamoja na wadau wengine.

Katika kutekeleza wajibu huo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilizindua Kliniki ya Kutoa Ushauri wa Kisheria pamoja na Kutoa Elimu kwa Umma. Kliniki hiyo ilizinduliwa rasmi katika Mkoa wa Dodoma mnamo tarehe 26 Juni, 2024 na aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji wa Mahakama ya Rufaa Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi.

Kupitia Kliniki hiyo Ushauri wa Kisheria na Elimu kwa Umma vinatolewa bure kwa wananchi wote wenye uhitaji. Ikumbukwe kuwa huu ni moja ya Mipango Mkakati wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, unaolenga kuwafikia wananchi katika Mikoa na Wilaya zote kwa kutumia Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria walio katika Mikoa na Wilaya husika kwa kushirikiana na Taasisi na Mamlaka mbalimbali katika sehemu hizo.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatoa rai kwa wananchi wote kuhudhuria katika Kliniki hizo, ambapo watapata fursa ya kuwasilisha changamoto mbalimbali za kisheria walizonazo na kupata fursa ya kushauriwa na kuelimishwa bure. Vievile kupitia Kliniki hizo kutakuwa na wasaa wa kutatua malalamiko ya kisheria ambayo yanawakabili wananchi kutokana na ukweli kuwa wananchi wengi hususani katika maeneo ya vijijni kushindwa kumudu gharama za kufika au kupata huduma au kukosa majibu kutoka kwenye Mamlaka husika. Sambamba na hayo, kliniki hizi zinasaidia wananchi kufahamu wapi watapata huduma.

Kliniki hizo zinalenga pia kuwajengea uwezo wananchi wa kuweza kuzijua haki zao na wajibu walionao katika kupata au kutafuta haki zao. Kliniki hizi zitasaidia kuokoa fedha nyingi za Serikali zinazotokana na tozo zinazotolewa dhidi ya Serikali katika Mahakama na Mabaraza ya Kimataifa.

Dhamira ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kutoa elimu na ushauri kwa wananchi ili kusikiliza, kutatua na kuepusha migogoro dhidi ya Serikali na miongoni mwa wananchi. Kupitia

kliniki hizo pia elimu ya sheria inatolewa kwa watendaji wa Serikali hususani katika Taasisi za Ardhi ambako kuna migogoro mingi isiyo ya lazima ambapo inaonyesha kuwa endapo sheria zingefuatwa katika hatua za Urasimishaji wa maeneo ili kupisha maendeleo au maslahi ya umma kama vile hospitali na shule na viwanja vya michezo, mingi ya migogoro hiyo ingeweza kuepukwa.

Kliniki hii ya Elimu na Ushauri wa kisheria mpaka sasa imeweza kuwafikia jumla ya wananchi **207** ambao wamepatiwa elimu, ushauri na huduma zingine za kisheria ambapo kati ya hao jumla ya malalamiko **145** yalipokelewa na kushughulikiwa. Malalamiko mengi yalikuwa yanahusiana na migogoro ya ardhi hususan wengi wao wakilalamikia kudhulumiwa ardhi zao na hivyo kupelekea kuchelewa au kukosa haki zao hasa wakati wa Urasimishaji wa maeneo yao.

Kliniki hizi ni endelevu na zinalenga kuwafikia wananchi wote kwa kutoa huduma hizi katika ngazi zote za Mikoa na Wilaya kupitia Kamati za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya. Kutakuwa na waratibu katika kila mikoa na wilaya watakaohakikisha huduma hizi zinafanyika mara kwa mara.

Aidha, katika kuhakikisha wananchi wananufaika na huduma ya kliniki ya Sheria,Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inahudumia wananchi kupitia namba ya Simu ya bure, Mwananchi anaweza kupiga simu hiyo ili kupata huduma za kisheria wakati wowote inapohitajika huduma hiyo ni ya bure. Namba ya simu hiyo ya simu ni **0800110188.**

**Mwandishi wa Makala hii ni Bi. Grace Komba, Wakili wa Serikali Mkuu (Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.)**